

HATI YA ZAWADI YA SHAMBA

KATI YA

**HALMASHAURI YA KIJJI CHA MWAVI
(MTOAJI)**

NA

**AFRICA STEEL GROUP COMPANY LIMITED
(MPOKEAJI)**

**KWA ZAWADI LA SHAMBA LILILOPO KITONGOJI CHA ZEMBA, KIJJI CHA
MWAVI KATA YA FUKAYOSI -BAGAMOYO LENYE UKUBWA WA EKARI 40**

HATI YA ZAWADI YA SHAMBA

Hati ya zawadi ya Shamba umesainiwa leo hii

Tarehe 13 Mwezi 05 Mwaka 2022.

KATI YA

HALMASHAURI YA KIJIKI CHA MWAVI, wa S.L.P 59, BAGAMOYO, Taasisi ya Kiserikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287, ambaye katika Hati hii ataitwa "**Mtoaji**", (jina ambalo litawahusisha warithi wake, wawakilishi, ndugu na jamaa zake) wa Upande Mmoja;

NA

AFRICA STEEL GROUP COMPANY LIMITED, wa S.L.P 8513 DAR ES SALAAM, Kampuni ambayo imesajiri kwa namba za usajili Na.155474521, ambae katika hati hii ataitwa "**Mpokeaji**", (ambayo itawahusisha warithi wake, wawakilishi, ndugu na jamaa zake) wa Upande wa Pili.

KWA KUWA Mtoaji ni mmiliki halali wa shamba, lililopo katika **kitongoji cha Zemba, Kijiji cha Mwavi, Kata ya Fukayosi** ndani ya Wilaya ya Bagamoyo ambalo katika Hati hii litaitwa "**SHAMBA**", ambalo lina ukubwa wa **Ekari 40** na Amehiyari kutoa shamba hilo kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda cha kutengeneza Nondo; shamba hilo lina majira ya nukta yafuatayo;

1. 458895	9293014
2. 458825	9292387
3. 459060	9292398
4. 459163	9292768
5. 459189	9292768
6. 459062	9292771
7. 459097	9292968

KWAKUWA, Mpokeaji ambaye Kampuni iliyosajiliwa kisheria imekubali kupokea zawadi ya shamba na kuhaadi kulitumie eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha nondo.

HIVYO BASI HATI HII UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:

1. Kwamba "**Mtoaji**" kwa upendo wa dhati na kwa hiyari yake ameamua kumpa zawadi la **SHAMBA** lenye ukubwa tajwa hapo juu "**Mpokeaji**";

2. Kwamba SHAMBA lilotolewa kama zawadi katika hati hii ni Mali ya "Mtoaji" na halina mkopo au mgogoro wowote katika vyombo vya kisheria.
3. Kwamba "Mtoaji" kuanzia tarehe ya kusaini hati hii SHAMBA lililotolewa kama zawadi litakuwa chini ya **Umiliki** wa "Mpokeaji" kisheria.
4. Kwamba "Mtoaji" anathibitisha kuwa zawadi ya SHAMBA alilotoa kwa "Mpokeaji" imezingatia ridhaa ya Mkutano Mkuu wa kijiji.
5. Kwamba Hati hii inatamka ya kwamba Shamba ni mali ya "Mpokeaji" kisheria;
6. Kwamba shamba linalotolewa na Mtoaji ni sharti litumike kwa shughuli za uwekezaji wa kiwanda cha Nondo na sio vinginevyo;
7. Kwamba Mpokeaji na Mtoaji wamekubaliana kuwa baada ya kiwanda kuanza kufanya uzalishaji kutakuwepo na makubaliano ya kusaidia jamii (Corporate Social Responsibility) kwenye masuala ya ajira, Maji Afya, Elimu na Mazingira.

KWA USHUHUDA pande zote mbili katika Hati hii zimesaini hati hii siku na tarehe inayoonekana hapa chini:

Kwa upande wa Halmashauri ya Kijiji cha Mwavi

Jina; Yahaya Omary Ally

Saini;.....

Cheo; Mwenyekiti wa Kijiji

Tarehe; 13-05-2022

Jina; Zahra Swalehe Iddi

Saini;.....

Cheo; Afisa Mtendaji wa Kijiji

Tarehe; 13-05-2022

Kwa upande wa AFRICA STEEL GROUP COMPANY LIMITED

Jina; XIAOYI ZHENG

Saini;.....

Cheo; Mkurugenzi wa Mtendaji

Tarehe; 13/05/2022

Jina; HONGTAO ZHENG

Saini;.....

Cheo; Mkurugenzi Mtendaji

Tarehe; 13/05/2022

